JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIAOFISI
YA RAIS TAMISEMI

Mawasiliano: **Shule ya Sekondari Kakonko,**
E-mail: jescamasawe2015@gmail.com **S.L.P 03**
Mkuu wa shule: 0755712846/0678458220Kakonko. **30.05.2022**

Makamu wa shule: 0757841015.
Mhasibu wa shule:0752931950.au 0755561440
Mtaaluma: 0768078372

Mzazi/Mlezi Wa Mwanafunzi .....
S.L.P……
…….

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KAKONKO YENYE MICHEPUO PCB,CBG,HGE,HGK,HGL NA HKL ILIYOKO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO, MKOA WA KIGOMA. MWAKA-2022.

1. .Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano mwaka 2022 Katika shule ya sekondari Kakonko, kwaTahasusi/mchepuo wa……..
Shule ipo umbali wa kilomita 1.5km Kusini mwa mji Mkuu wa Wilaya ya Kakonko. Usafiri wa bodaboda kutoka kituo cha mabasi Kakonko ni nauli **Tsh.1000/=**

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **……..** Unatakiwa kuripoti Shuleni kuanzia tarehe **……**mwisho wa kuripoti ni **…….**

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia.**

2.1 Sare ya shule

RANGI YA SARE YA SHULE

2.1.1 Wasichana

a) Sketi mbili rangi ya bluu nyeusi(dark blue kitambaa cha suti) yenye urefu hadi kwenye **kisigino** na isiyo bana yenye **mshono wa malinda mkeketo nchi** $1\frac{1}{2}$**,** hii ni Sare ya **darasani** (Siketi hizo zinapatikana shuleni kwa bei ya Tsh.18000/= kwa kila moja).

b) Nguo za kushindia (shamba dress) ni sketi mbili za rangi ya zambalao (purple kitambaa cha suti), mshono **wa malinda mkeketo nchi** $1\frac{1}{2}$. (Siketi hizo zinapatikana shuleni kwa bei ya Tsh.18000/= kwa kila siketi moja).).

c)Shati mbili nyeupe zenye mikono mirefu zisizo na mapambo yoyote wala zisibane.

d) Soksi nyeupe jozi mbili.

e) Viatu vyeusi vya ngozi vinavyofunika miguu, **vyenye Kamba**, na visigino vifupi.

f) T-shirt za shule mbili atazikuta shuleni kwa gharama ya T-shs 20000/=

g) Bajaji/simplena yeboyebo haziruhusiwi shuleni kabisa.
h) Nguo nyingine zozote mbali na sare zilizotajwa hapo juu **haziruhusiwi**.
i) kwa wa Islamu ataruhusiwa kuvaa Hijabu nyeupe darasani na Hijabu ya rangi ya Zambalau (purple) kama vazi la kushindia, zishonwe kwa kufuata maelekezo ya serikali.(ziishie usawa wa kiwiko)

2.1.2 Wavulana:

a) Suruali mbili za bluu nyeusi (dark blue) za darasani zenye mifuko mitatu. Suruali zote lazima ziwe na marinda, tanapu ya chini na ziwe na upana wa chini 17cm. **(SURUALI ZA MODEL HAZIRUHUSIWI).** (Suruali hizo zinapatikana shuleni kwa bei ya Tsh.16000/= kwa kila moja)
b) T-shirt mbili za shule utazikuta shuleni kwa Tshs 20000/=
c) Tai mbili za dark blue(zinapatikana shuleni Tsh 2000 kila moja)
d) Shati mbili nyeupe zenye mikono mirefu zisizo na mapambo yoyote wala zisibane.
e) Soksi nyeusi jozi mbili.
f) Nguo za kushindia(shamba dress) ni suruali mbili za rangi nyeusi zenye mifuko mitatu.Na suruali zote lazima ziwe na marinda, tanapu ya chini na ziwe na upana wa chini 17cm. **(SURUALI ZA MODEL HAZIRUHUSIWI).** (Suruali hizo zinapatikana shuleni kwa bei ya Tsh.16000/= kwa kila moja)
g) Viatu vyeusi vya ngozi vinavyofunika miguu, vyenye Kamba, na visigino vifupi.
h) Bajaji na yeboyebo haziruhusiwi kabisa.
i) Nguo nyingine zozote mbali na sare zilizotajwa hapo juu **haziruhusiwi**.
j) Aje na ndala za kuogea na viatu vya kushindia.

2.1.3 Sare za Michezo

Sare za michezo kwa shule hii ni kwa wote yaani wavulana na wasichana.
a) Raba za michezo kwa wanafunzi wote
b) Bukta rangi ya bluu kwa wavulana na **full tracksuit** kwa wanafunzi wote rangi ya bluu-bahari yenye mchirizi mweupe.

2.2 Ada na Michango ya Shule

(a) Ada ya shule kwa mwaka ni Shilingi **70,000/=,** nusu muhula ni shilingi **35,000/=**
Fedha hii ilipwe **NMB A/C NO.51501100051** yenye jina la **KAKONKO SECONDARY SCHOOL CONTRIBUTION ACCOUNT**

(b) **Michango inayotakiwa kulipwa kwa kila mzazi/ mlezi:-**

S/N	AINA YA MCHANGO	KIASI
1	Ukarabati wa samani	15,000
2	Kitambulisho	6,000
3	Taaluma	20,000
4	Watumishi wa shule(wapishi,walinzi,na vibarua wengine)	35,000
5	Nembo ya shule	3,000
6	Mtihani wa mock	25,000
7	Huduma ya kwanza na bima (CHiF)@5000	10,000
8	Tahadhari	5000(haitarejeshwa)
	Jmla michango	118,000
	JUMLA KUU IKIWEMO NA ADA KWA MWAKA	188,000/=

Michango hiyo ilipwe kupitia account ya shule JINA: *KAKONKO SECONDARY SCHOOL* CONTRIBUTION ACCOUNT. NAMBA: (51501100051) NMB.
Jumla ya ada na michango yote kwa mwanafunzi ni shilingi laki moja na elfu themanini na nane tu (Tsh 188,000/=) N:B;
Kwa mawasiliano yeyote yatakuwa kati ya uongozi wa shule kwa namba za simu hapo juu.
Na pia mwenye BIMA YA NHIF hatalipa sh.5,000/= ya CHiF,hivo yeye jumla atalipa sh.183,000/=

Shule ina umeme wa TANESCO ila mwanafunzi anashauriwa kuja na taa ya solar au tochi kwa matumizi yake pale UMEME unapokatika..

(c) **Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

i. Kila mwanafunzi aje na Ream 2 (kwa mwaka) – (Karatasi A_4 aje nayo mkononi). ii. Godoro utalikuta shuleni kwa malipo ya Tshs.elfu ishirini (20000/=) kwa mwaka, NB.Fedha hiyo ya godoro italipwa mara moja siku utakayo ripoti **.** iii.Mwanafunzi aje na bedcover rangi ya darkblue kitambaa cha kotoni (foronya ya godoro) size ya futi $2\frac{1}{2}$ x 6.

iv. Mashuka mawili, moja la **blue na pinki moja aje nayo**.

v. Madaftari makubwa 10 (counter book quire 3 au 4 kwa ajili ya kuandikia matini (Notes) ya masomo. vi. Mkebe wa hisabati, na kikokotozi cha kisasa (**Non-programablescientific calculator fx 991**) kwa Wanafunzi wa sayansi. vii. Wanafunzi wa arts waje na kamusi ya kiingereza na Kiswahili (Advanced Dictionary.) viii. Rula, kalamu na penseli kwa wanafunzi wote. ix**.** Kitabu kimoja cha rejea na kiada kwa kila somo. **Hivyo vitabu vitakuwa mali binafsi ya Mwanafunzi .**

x. Kila mwanafunzi aje na tranka imara la kutunzia vitabu vyake.

xi.Kila Mwanafunzi aje na vyomba vya chakula yaani Sahani moja, Bakuli moja, Kikombe na Kijiko.

xii. Kila Mwanafunzi wa kike na wa kiume aje na (jembe moja lenye mpini) , fyekeo 1, ndoo mbili(2) za lita kumi,beseni moja(1) , kidumu kimoja (1)cheupe cha lita tano kwa ajili ya maji ya kunywa ,ufagio wa chelewa mmoja(1),soft au hard broom (brush) moja(1),na mopa/squeezer moja(1). xiii. Mwanafunzi wa PCB na CBG aje na dissecting kit , mwanafunzi wa HGL aje na kamusi ya kingereza,HKL aje na kamusi ya kingereza na kiswahili,HGK aje na kamusi ya kiswahili.

NB: Mambo ya Kuzingatia Shuleni.

i. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.

ii. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

iii. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka wakati wote wa uanafunanzi wako katika shule hii. (**huduma nyingi zinapatikana kwenye duka lililopo ndani ya shule).**

iv. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.

v. Kuvaa sare ya shule wakati wote uwapo shuleni na nje ya shule pale unapokuwa kwenye shughuli za kitaaluma na ama shule.

vi. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote. vii. Sare za shule huvaliwa wakati wote ukiwa Shuleni, wakati wa kwenda nyumbani na wakati wa kurudi shuleni.

viii. Lugha ya mawasiliano uwapo shuleni kwa muda wote ni Kiingereza.

ix. Wanafunzi wote wa kike na wa kiume wanyoe nywele urefu wa sentimita moja (1) zinazofanana kichwa kizima.

11. **3.MAKOSA YA KUWEZA KUKUFUKUZISHA SHULE**

i. Wizi ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini bila taarifa/utoro

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu,walezi na jamii kwa ujumla.

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu, au mtu yeyote Yule.

vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wako shuleni

vii. Kufuga nywele na ndevu viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya ix. Uvutaji wa sigara.

x. Uasherati,uhusiano wa jinsi moja,kuoa au kuolewa. xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba xii. Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yanayovunja sheria za nchi.

xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

xv. Kumiliki,kukutwa au kutumia **simu ya mkononi** au kukutwa na **chaja ya simu** katika mazingira ya shule

xvi. Kudharau bendera ya taifa

xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu xviii. Uharibifu wa mali ya uma kwa makusudi

4. Viambatisho na Fomu Muhimu.

a) Medical Examination form ambayo itajwa na Mganga Mkuu wa hosipitali ya selikal. Fomu hii imeambatishwa na barua hiii

b)Fomu ya maelekezo binafisi kuhusu historia ya mwanafunzi mkataba wa kutoshiriki katika mgomo,fujo na makosa ya jinai.

c)Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni kulipa ada,michango na maelekezo mengine yaakayotolewa na shule.

5. Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza.

KARIBU SANA KAKONKO SEKONDARI

ELIMU BORA KWA MAENDELEO YA JAMII

JESCA C.MASAWE

MKUU WA SHULE.

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KAKONKO

HISTORIA YA MWANAFUNZI.

1. Jina la mwanafunzi……..
2. Jina la baba ……..
3. Jina la mama……
4. Jina kamili la mlezi……..
5. Anuani ya mzazi/mlezi…… 6. Uhusiano wa mlezi……...
7. Kazi ya baba (mkulima, mfanyabiashara, mfanyakazi) 8. Kama ni mkulima zao muhimu analolitegemea ni……..
9. Kama ni mfanyabiashara, biashara yake ni.....
10. Kama ni mfanya kazi, kazi yake ni……
11. Afya ya mwanafunzi, Kama anayo matatizo ya kiafya na hivyo kustahili huduma maalum. Tafadhali mzazi/mlezi aeleze wazi

……
……
……
12. Madhehebu ya dini……
13. Jamaa na ndugu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya mzazi/mlezi.

Jina kamili Kazi yake Anuani yake (Simu)

1. …….. ……. …… 2. …….. ……. ……....
3. …….. ……. …….....
4. …….. ……. ……

KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE.

Jina la mwanafunzi…… Jina la mzazi/mlezi……...
Anuani ya mzazi/mlezi……..
Uhusiano……...….(mjomba, shangazi, kaka, dada). Mimi ……nikiwa nimechaguliwa kuwa mwanfunzi wa Tanzania naamini kuwa nimetunukiwa nafasi hiyo niliyopewa na umma wa Tanzania.
Hivyo naahidi kuwa nitajibidiisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zote nitakazopewa hapa shuleni nje na ndani ya darasa ili kuleta ufanisi.
Ili kutimiza shabaha hiyo ninakubali na ninaahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitafanya kazi kwa BUSARA, JUHUDI YA HALI YA JUU KABISA NA KUTII kwa viongozi wote wa shule pamoja na sheria. Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia na taratibu zinazokubalika.
Sahihi ya mwanafunzi……Tarehe…….....
Mimi ……mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……..ninaahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wa mtoto huyo kwa kushirikiana na shule.
Sahihi ya mzazi/mlezi……Tarehe…… Page 7 of 11

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.

Pupil's name……...

Age ……

Stool test……

Blood group……...

Urine analysis……. Sphills test ……....

Chest test……

Speech…… Eye test …….

Abdomen……

Additional information and physical defect or impairment to pursue further education

……

……..……

……

Signed ……

Designation ……

Official stamp

Date ……

OFISI YA RAISI
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
TAMISEMI.
SHULE YA SEKONDARI KAKONKO.
AHADI YA MZAZI:

Mimi……(Jina kamili) ambaye ni mzazi/mlezi wa ……..kidato cha…….

Nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema.Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii.Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia mwanangu malezi na elimu bora kwa manufaa ya Taifa la Tanzania.Na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapo takiwa kufanya hivyo.Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria,kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

Saini ya mzazi/mlezi…….

Anuani kamili……

Simu……

Tarehe…….